



34 Yohana Mbaptizaji

Kwa Biblia Luka 1:5-23, 57-66 na 80

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba tunatakiwa tuamini chenye Mungu anasema

Somo

Wakati wa Agano la Kale, Mungu alituma manabii wengi kufundisha watu. Manabii wengi waliandika chini maneno ya Mungu. Haya maneno yameandikwa ndani ya Biblia yetu kwa Agano la Kale. Mungu aliahidi kwamba siku moja atatuma mfalme wa ajabu. Ahadi za Mungu ziliandikwa chini. Wayahudi walisoma maneno ya manabii. Walizijua hizo ahadi za Mungu. Wayahudi walikuwa wakimngojea Mfalme (Masihi) aje. Walikuwa wameongoja kwa muda mrefu. Wayahudi wengine walikuwa wamechoka kuongoja. Mungu alitaka Wayahudi wajitayarishie Masihi wao. Mungu alituma nabii mwingine awambie kwamba Masihi anakuja hivi karibuni. Huyu nabii alitwa Yohana mbatizaji.

Kulikuwa na kuhani aliyetwa Zakaria. Alikuwa na mke jina lake Elisabeti (binamye Mariamu – unakumbuka kwa somo lililopita Mariamu alienda kuona Elisabeti). Zakaria na Elisabeti walikuwa wote wazee. Hawakukuwa na mtoto. Sasa walikuwa wazee sana, hawangeweza kupata watoto.

Siku moja Zakaria alikuwa anafanya kazi kwa Hekalu. Alikuwa amechaguliwa kwenda Pahali Patakatifu kufukizia Mungu uvumba. Papo hapo malaika alimtokezea. Malaika alisimama upande wakulia wa madhabahu ya uvumba.

Maswali

1. Jina la mke wa Zakaria lilikuwa nani?
2. Zakaria na Elisabeti walikuwa wazee sana kufanya nini?
3. Zakaria aliona nini kwa Hekalu?
4. Malaika Gabrieli aliambia Zakaria nini?
5. Zakaria aliamini malaika?
6. Malaika alipea Zakaria ishara gani?
7. Elisabeti alisema ni lazima mtoto aitwe nani?
8. Nini ilifanyika baada ya Zakaria kuandika, “Jina lake ni Yohana?”
9. Yohana alipokua mkubwa alienda kuishi wapi? Alikula nini?
10. Mungu alikuwa amechagulia Yohana kazi gani?

Majibu

1. Mke wa Zakaria aliitwa Elisabeti.
2. Zakaria na Elisabeti walikuwa wazee sana kupata mtoto.
3. Zakaria aliona malaika kwa Hekalu.
4. Malaika alisema kwamba Zakaria na Elisabeti watapata mwana.
5. Hapana. Zakaria alisema walikuwa wazee sana kupata mwana.
6. Malaika alisema kwamba Zakaria atakuwa bubu mpaka mtoto azaliwe.
7. Elisabeti alisema kwamba lazima mtoto aitwe Yohana.
8. Zakaria aliweza kuzungumza tena.
9. Yohana alienda kuishi jangwani. Alikula nzige na asali ya mwituni.
10. Mungu alichagua Yohana kuwa nabii, kuambia watu kwamba Masihi anakuja.

Malaika aliambia Zakaria, “Usiogope. Mungu amesikia maombi yako. Utakuwa na mwana. Lazima umuite Yohana. Atakuwa wa furaha kwako. Atakuwa nabii wa ajabu kama Eliya. Ataleta watu wengi kwa Bwana Mungu wao. Atafanya watu wawe tayari kupokea Masihi.”

Zakaria hakuamini kwamba yeye na Elisabeti vile wako wazee wanaweza kupata mtoto. Zakaria aliuliza malaika, “Nitajuaje kwamba haya yatakuwa ya kweli.” Malaika alijibu Zakaria, “Mimi ni malaika. Jina langu ni Gabrieli. Mungu amenituma nikwambie habari hizi njema. Mungu atakupata ishara kwamba ni kweli. Utakuwa bubu. Hautaweza kuzungumza tena mpaka mtoto atakapozaliwa kwa sababu haukuamini maneno yangu.”

Watu walistaajabu mbona Zakaria alikawia ndani ya hekalu. Zakaria alipotoka hekaluni alikuwa bubu. Zakaria alikuwa bubu na hangeweza kuambia watu nini ilitendeka. Zakaria alitumia ishara kwa kuambia watu kwamba ameona malaika. Lakini hakuwambia ni nini malaika alisema.



Maneno ya malaika ilikuwa ya kweli. Elisabeti alipata mimba. Alipata mtoto mvulana. Majirani na watu wa jamii walifurahia mtoto mweye Elisabeti alizaa. Alikuwa mtoto asiye wa kawaida. Kwa sababu mtoto aliahidiwa na Mungu tena alizaliwa wakati Zakaria na Elisabeti wako wazee.

Siku ya nane ilikuwa ya kuita mtoto jina. Kila mtu alisema, “Tutaita huyu mtoto ‘Zakaria’ jina la baba yake.” Lakini Elisabeti alisema, “Hapana! Ataitwa ‘Yohana.’” Jamii ya Elisabeti walisema, “Hakuna mtu kwa jamii yenu anayeitwa kwa jina hilo.” Zakaria alikuwa bado bubu. Walimfanyia ishara wakimuuliza ni jina gani atapenda waite mtoto. Zakaria aliandika kwa kibao, “Jina lake ni Yohana.”

Papo hapo Zakaria akaanza kuzungumza tena. Alisifu Mungu kwa uzuri wake. Majirani wote na jamii walistaajabu kwa haya yote. Walishangaa na kujiuliza Yohana atakua akiwa mtu wa aina gani. Walijua Mungu alikuwa naye.

Mungu alikuwa amechagua Yohana kuwa nabii wa kipekee. Akikua mkubwa atakuwa nabii wa Mungu. Yohana ataambia watu wote kwamba Masihi wa Mungu atakuja hivi karibuni.

Yohana alipokua alienda kuishi jangwani. Alivaa kanzu ya ngozi na singa za ngamia. Alikula nzige na asali ya mwitu. Yohana aliishi jangwani kwa muda. Alikuwa akijitayarisha kuwa nabii wa Mungu. Halafu Mungu akamwambia aende na aambie watu wote kwamba Masihi anakuja.

